

Utandawazi kama Tisho kwa Lugha za Kiafrika

Mosol Kandagor na Toboso Mahero

Ikisiri

Ulimwengu una lugha takribani elfu sita. Hata hivyo, nyingi katika lugha hizi zimo katika hatari ya kuangamia. Inasemekana kwamba lugha moja ya ulimwengu huangamia katika majuma mawili. Nchini Kenya, lugha za Kisengwer, Kisuba na Kielmolo zimo katika hatari ya kuangamia. Ingawaje lugha nyingi za ulimwengu zinakabilwa na changamoto za kuishi, Kiswahili kimo mbioni kukua na kupanuka. Sasa hivi, Kiswahili kimekuwa lugha ya ulimwengu na kinatekeleza majukumu muhimu ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Usambaaji wa kasi wa Kiswahili katika eneo la Maziwa makuu Afrika unatokana na mazingira mvafaka ya ukuaji ambayo yamekuwepo tangu wakati kabla ya ukoloni wa mataifa ya Afrika Mashariki. Makala hii inachunguza utandawazi unavyotishia uwezo wa lugha za Kiafrika. Lugha zinazoangamia zimeanishwa katika makundi matatu - lugha zilizoangamia, lugha zilizolala na lugha zilizo katika hatari ya kuangamia. Athari za utandawazi kwa ubai, usambaaji na matumizi ya lugha mbalimbali ulimwenguni zimejadiliwa kwa kuangazia nyanja za elimu, uchumi, mawasiliano, siasa na hata utamaduni. Hoja inayojengwa ni kwamba jitihada za makusudi zinapaswa kutekelezwa ili kuzinusu lugha za Kiafrika zinazokabilwa na tishio la maangamizi. Imebainika kwamba ubijadhi wa lugha ni muhimu kwa kuwa lugha huwasilisha utamaduni, hutambulisha na, ni sehemu muhimu ya amali za watu.

Maneno Muhimu: *Utandawazi, Lugha, Kenya, Jamii*

Utangulizi

Takribani lugha moja ya ulimwengu huangamia kila baada ya majuma mawili. Mintarafu ya UNESCO (2010) lugha 200 za ulimwengu zimeangamia katika vizazi vitatu vilivyopita ilihali lugha 632 zimo katika hatari kubwa ya kuangamia. Lugha kati ya 4,000 na 6,000 zimeangamia tangu karne ya 15 (Garrick & People, 2003). Nchini Kenya, kuna lugha kati ya 30 na 60 (Batibo, 2005; Githiora, 2006 na Heine & Mohlig, 1980), na 13 kati ya lugha hizi zimo katika tisho la kuangamia (Batibo, keshatajwa). Mintarafu ya uchunguzi wa UNESCO (2010), asilimia 10 ya lugha 2000 za Kiafrika zitaangamia katika miaka ijayo 100. Hii ina maana kwamba asilimia 10 ya kizazi kijacho huenda wasiwe na uwezo wa kuzungumza lugha mama yao. Baadhi ya lugha hizi nchini Kenya ni Kisengwer, Kielmolo na Kisuba. Hii haimanishi kwamba lugha za Kiafrika zilizosalia ziko salama. Shirika la UNESCO (UNESCO, 2010), limebainisha Kenya kuwa ni taifa lililo na hatari kubwa mno ilihali Kenya ina lugha sita zilizoangamia na nyingine kadhaa kuwa katika tisho. Uganda imepoteza lugha mbili pekee ilihali asilimia kubwa ya lugha za Tanzania, Rwanda na Burundi zingali salama (Otieno, 2010). Hata hivyo, lugha za mataifa haya huenda zikawa katika hatari hivi karibuni iwapo hatua za dharura hazitachukuliwa.

Baadhi ya lugha zimekwisha kuangamia. Mathalani, umoja wa Mataifa umebainisha Kiyakunte kama mojawapo ya lugha ambazo zimekwisha kuangamia (UNESCO, 2010). Kwa mujibu wa ripoti hii, lugha za Kisogoo, Kielmolo, Kinare, Kikore na Kilorkoti zimekwisha kuangamia. Obiero (2008) anaongezea kwamba lugha za Kiong'om, Kiburji, Kidahalo, Kidegere, Kiterik, Kinare, Kikore, Kiomotik, Kisegeju, Kiboni na Kisuba nazo zimo mbioni kufikia mauti yake. Mintarafu ya Osman (Aljazeera, 2018), wazee kumi pekee Wayaaku ndio walio na uwezo wa kuzungumza lugha mama yao ya Kiyakunte.

Kuna dalili nyingi za kudidimia kwa lugha kwa sababu anuwai ikiwemo mtagusano wa lugha (Brenzinger, 1992; Batibo, 2005). Lugha nyingi za Kenya zinadidimia kutokana na sababu tofautitofauti. Kwanza, ni sababu za kikoloni. Wayaaku kwa mfano, walisimilishwa na Wamaasai baada ya Wamaasai, ambao ni jamii kubwa, kuingia katika maaazi yao ya msitu wa Mukogodo na kuanza kuishi mle. Wayaaku hatimaye walisimilishwa na kuanza kuzungumza Kimaasai. Sasa, Wayaaku wanachukuliwa na serikali ya Kenya kuwa sehemu ya jamii ya Wamaasai. Kabla ya ukoloni, Kisuba kilikuwa lugha kuu. Mintarafu ya UNESCO (2010) wazungumzaji wa Kisuba walikuwa takribani 200,000 mnamo mwaka wa 1992 lakini sasa hivi kimebainishwa kuwa ni lugha inayoelekea kufariki. Kwa sasa, lugha hii inazungumzwa katika maeneo machache tu kama visiwa vya Mfangano na Rusinga na Gwasi (Otieno, 2010).

Kutokana na usuli huu, makala hii inachunguza jinsi ambavyo utandawazi unatishia uwepo wa lugha asili za Kiafrika. Inaanza kwa jaribio la kuainisha lugha zinazoangamia katika makundi mbalimbali kisha kuonyesha namna utandawazi unavyotishia kua lugha za Kiafrika. Sehemu inayofuata inajadili athari za utandawazi kwa lugha na kueleza dhima ya kuhifadhi lugha za Kiafrika. Hatimaye, njia za kuhifadhi lugha zimefafanulia kabla ya hitimisho kutolewa. Uhifadhi wa lugha umedhihirika kuwa muhimu kwa sababu lugha huwasilisha utamaduni, ni kitambulisho na sehemu muhimu ya amali za jamii zinazohusika.

Uainishaji wa Lugha Zinazoangamia

Lugha zinazoangamia zinaweza kuainishwa katika makundi matatu. Kwanza, kuna lugha zilizoangamia. Lugha isiyo na mzungumzaji yeyote huchukuliwa kuwa lugha iliyoangamia (Crystal, 2000). Kadhalika, lugha zisizotumika na ambazo hazina rekodi ya maandishi, huchukuliwa kuwa lugha zilizoangamia (Crystal, keshatajwa). Kuna sababu anuwai za kuangamia kwa lugha. Iwapo lugha haitakuwa na wazungumzaji wanaoweza kuipokeza kwa kizazi kijacho, basi kuna hatari kubwa ya lugha hiyo kuangamia. Iwapo wazungumzaji wa lugha fulani hawana mazingira yanayofaa kujiendeleza kiuchumi, kuna hatari ya lugha ya jamii hiyo kuangamia kutokana na sababu za kiuchumi (Nettle & Romaine, 2000). Aidha, iwapo kundi la wazungumzaji wa lugha halina imani kwamba lugha yao haina upekee wa kuwatambulisha wao kama jamii, kuna hatari ya jamii hiyo kupuuzwa lugha yao na kusababisha maangamizi yake (Singh & Jones, 2005).

Pili, kuna lugha zilizolala. Hili ni kundi la lugha zisizo hai wala hazijafa. Hizi ni lugha zisizo na wazungumzaji na hivyo, hazitumiwi katika mawasiliano wala shughuli yoyote ya kimazungumzo. Ni maneno machache tu ya hizi lugha ndiyo yanayotumika. Lugha hizi huwa na rekodi ya maandishi ambayo inaweza kutumiwa kuzifufua na kuzileta katika matumizi yake ya awali. Mifano ya lugha hizi ni lugha ya Miami ambayo ilikuwa imelala miongo mitano iliyopita lakini sasa inafufuliwa na imeanza kutumika katika jimbo la Oklahoma, Marekani (Leonard, 2008).

Tatu, kuna lugha zilizo katika hatari ya kuangamia. Lugha iliyo na mzungumzaji mmoja tu huchukuliwa kuwa katika hatari ya kuangamia (Crystal, 2000). Lugha zinazotumika kwa nadra, kama vile katika sherehe za elimu au za kidini pekee bali hazitumiki katika mawasiliano ya kawaida huchukuliwa kuwa lugha zilizo katika hatari ya kuangamia. Hata hivyo, lugha hizi huwa na uwezo wa kuendelea kuishi na pia zina uwezo wa kufufuka na kuanza kutumika katika mawasiliano ya kawaida. Mfano wa lugha hizi ni Kiyunani, Kislovani, Kikopti, Kihebrania na Kilatino (Wurm, 1991). Matalani, nchini Israeli, kuna ongezeko la matumizi ya Kihebrania katika mawasiliano ya kila siku, japo kwa muda mrefu, lugha hiyo imetumika katika misingi ya dini pekee (Nettle & Romaine, 2000).

Utandawazi na Kifo cha Lugha za Kiafrika

Utandawazi ni mchakato wa muungano wa mataifa ya ulimwengu unaotokana na kubadilishana kwa mawazo, mwonoulimwengu, elimu, bidhaa na utamaduni (Nayef & Stoudmann, 2006). Utandawazi pia unaweza kufafanuliwa kama mtandao mkubwa unaohusisha mitagusano ya kiuchumi, kijamii, kitamaduni na kisiasa inayovuka mipaka ya nchi (Yeates, 2001; Wells, 2004; Robb, 2007; Hufbauer & Suominen, 2010; Muller, 2010) na husababisha kutegemeana kwa watu wa ulimwengu (UNDP, 1999). Utandawazi sasa umemeza ulimwengu mzima chanzo chake kikiwa mchakato wa kibepari wa karne nyingi (Glazter & Rueschemeyer 2005). Hii ndiyo sababu lugha kuu za kibepari zimeandamana nao, huku lugha zisizo za kibepari zikiangamia au kutishiwa kuangamia. Mchakato wa utandawazi umesababisha ongezeko la mabadilishano yanayofanya ulimwengu kuwa taifa moja. Kwa sababu hii, utandawazi umefanya ulimwengu kubagua lugha na kukumbatia zile zilizo kuu na zenye uwezo wa kufanikisha haraka mchakato wake.

Umoja wa jamii huwa na mitagusano ambayo huhusisha lugha. Utandawazi umeleta mitagusano ya ulimwengu wote katika biashara, teknolojia, mawasiliano, elimu, utamaduni na hata siasa. Kutokana na mitagusano hii, lugha za Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu zimechukua nafasi ya mbele kama lugha za ulimwengu (Li, 2002; Corbin, 2007). Hali hii inaacha lugha zisizo na nafasi katika mchakato huu katika hali tata na hii ndiyo sababu umoja wa mataifa unasema kwamba asilimia 50 ya lugha na lahaja za ulimwengu huenda zikaangamia katika miaka michache ijayo kwa kuwa sasa, lugha moja inaangamia kila baada ya majuma mawili (UNESCO, 2012). Lugha nyingi za Kiafrika zimo katika

kundi hili la maangamizi. Ni lugha chache mno za Kiafrika zilizo na nafasi katika mchakato wa utandawazi. Miongoni mwa lugha hizi ni Kiswahili kwa kuwa sasa Kiswahili ni lugha inayotekeleza majukumu mengi kimataifa ikiwemo katika elimu, biashara na siasa. Lugha nyingine za Afrika Mashariki zimesalia katika hali tete na huenda nyingi zikakabiliwa na kifo chake katika miaka michache ijayo.

Utandawazi Unavyoathiri Lugha

Athari za utandawazi kwa lugha ni nyingi na zinadhihirika katika njia anuwai. Uchumi wa ulimwengu sasa umekuwa mmoja kwa kuwa mataifa yanategemeana. Hii ndiyo sababu taifa moja linapoporomoka kiuchumi, mataifa mengine pia huathirika. Mijadala ya kimataifa kuhusu uchumi huendeshwa katika lugha ya Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu kwa kuwa hizi ndizo zinazochukuliwa kuwa lugha za uchumi wa ulimwengu. Kutegemeana kwa uchumi wa ulimwengu hudhihirika katika makampuni ya kimataifa. Makampuni haya kutumia lugha za kigeni, hata wakati yanapowekeza katika mataifa ya kigeni. Mijadala ya kimataifa kuhusu uchumi pia hufanyika katika lugha kuu zinazochukuliwa sasa kama lugha za uchumi wa ulimwengu. Hali hii imeziacha lugha hizi katika hali hoi na hatari ya kuangamia.

Kuhusu siasa, ulimwengu mzima sasa unakumbatia siasa za demokrasia. Mataifa sasa yanabadilishana sera za kukuza siasa za demokrasia. Kidiplomasia, mataifa hutagusana kwa kubadilishana mabalizi. Katika hali hii, panahitajika lugha ya kufanikisha mawasiliano kati ya watu wa mataifa yanayopokea mabalizi hawa na wageni wao. Lugha zinazotumika hapa si lugha za Kiafrika bali zile za Magharibi. Lugha za Kiafrika sasa zinajikuta katika hali ya mapuuza katika siasa za kimataifa.

Utandawazi umesababisha maenezi ya elimu ya Kimagharibi ulimwenguni kote. Katika bara la Afrika, mataifa mengi yamechukua lugha za kigeni kuwa lugha za mafundisho shuleni. Wataalamu pia huathiriwa na suala la lugha. Mathalani, machapisho mengi huwa katika lugha za mafundisho ambazo nyingi ni za kigeni. Kwa sababu hii, wataalamu wa Kiafrika, kwa nia ya kutaka kuchangia mijadala ya kimataifa na elimu, huchapisha katika lugha za mafundisho ambazo nyingi ni za kigeni. Li (2002) anashuhudia hili anaposema kwamba Kiingereza sasa kimekuwa lugha ya sayansi ya ulimwengu na ndiyo lugha kuu inayotumiwa na wataalamu kuchapisha tafiti zao za kisayansi.

Utandawazi umesababisha maenezi ya sayansi, teknolojia na maarifa kuhusu teknolojia (Guerrieri, 1999; UNCTAD, 2001; Archibugi & Lundvall, 2001). Sasa, teknolojia imekuwa msingi wa maendeleo ya ulimwengu mzima. Kila teknolojia inayovumbuliwa huhitajika katika mataifa yote ya ulimwengu kwa kuwa mataifa yanategemeana. Nyingi katika ya teknolojia zinazovumbuliwa hutoka katika mataifa ya Magharibi na Asia. Teknolojia hii inaposambaa huambatana na majina asilia ambayo huwa katika lugha za Ulaya ilikovumbuliwa. Teknolojia hii pia huambatana na maelekezo kuhusu matumizi yake ambayo huwa katika lugha ya wavumbuzi, na tafsiri yake katika lugha za Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu. Kwa hivyo, matumizi ya teknolojia hii hutegemea lugha hizi. Hali hii imewacha lugha za Kiafrika katika mapuuza.

Utandawazi pia umesababisha uhamiaji wa watu. Uhamiaji umesababishwa na kutegemeana kwa mataifa kiuchumi na kijamii. Udhaifu wa mataifa ya Kiafrika kiuchumi umesababisha kuhama kwa raia wa mataifa ya Kiafrika kwenda katika mataifa yaliyostawi kusaka afueni katika maisha. Kuna pia sababu za kibiashara zinazosababisha kuhama kwa Waafrika kwenda katika mataifa mengine kujiendeleza. Sababu nyingine ni kama vile vita, dini na elimu. Kuhama kwa Waafrika kwenda katika mataifa mengine kumechangia kupunguka kwa wazungumzaji wa lugha za Kiafrika kwa kuwa baadhi ya wahamiaji hupata uraia wa mataifa yanayowapokea. Wengine wasiopata uraia wa huko huchukua lugha za mataifa hayo kama lugha kuu za mawasiliano yao huku wakipuuza lugha mama zao.

Utandawazi umesababisha mawasiliano mapana kati ya watu wa ulimwengu. Mitagusano katika elimu kati ya wanafunzi na wataalamu, biashara, dini na utalii imesababisha kuenea kwa matumizi ya lugha kuu za ulimwengu. Mawasiliano haya hupitia kwa maandishi au mazungumzo. Mawasiliano mengi ya kimataifa yaliyo katika maandishi kwa mfano barua pepe, huendeshwa katika lugha za kigeni, hata iwapo ni kati ya watu wa jamii moja. Lugha za Kiafrika pia zimeathirika katika mawasiliano ya mitandao. Mitandao mingi ya kijamii pia imezuka. Mawasiliano mengi katika mitandao hii yanaendeshwa katika lugha za kigeni. Mitandao yenyewe pia inatumia lugha za kigeni

kama lugha za maagizo ya mitandao yenyewe. Mathalani, mawasiliano mengi katika *Facebook* yanashirikisha Kiingereza na lugha nyingine za utandawazi (Toboso na wenzie, 2016 na Toboso, 2021). Kwa sababu hii, lugha za Kiafrika hukosa fursa ya kushiriki katika mawasiliano kwa sababu ya kupigwa kumbo na lugha za utandawazi.

Ukuaji wa miji ni sifa muhimu ya utandawazi (Jennings, 2011). Ukuaji wa miji tangu enzi ya mfumuko wa viwanda umesababisha kuhama kwa watu kutoka vijijini hadi katika maeneo ya miji. Athari ya miji kwa lugha za Kiafrika ni kwamba lugha za mawasiliano mapana ndizo huchukua hatamu ya mawasiliano ya mijini kutokana na changamoto za mawasiliano ya watu kutoka jamii nyingi. Miji imekuwa sababu kuu ya uhamaji lugha kwa kuwa watu wengi wanaohamia mijini pia huhama lugha zao na watoto wengi wanaozaliwa mijini hukosa uwezo wa kuzungumza lugha mama za wazazi wao kwa sababu ya changamoto za urithishaji lugha.

Dini pia zimeathiriwa na utandawazi. Haja ya kutaka kuwasiliana na hadhira ya waumini kimataifa imesababisha wahubiri kuendesha ibada zao katika lugha za kigeni. Sasa, si nadra kupata mahubiri maabadani yakiendesha katika Kiingereza, Kifaransa au Kiarabu. Makanisa sasa yamekuwa ya kimataifa huku yakilenga hadhira pana ya kimataifa. Baadhi ya makanisa pia yana ibaada zinazopeperushwa katika vyombo vya habari kama runinga na mwengoya. Ibaada nyingi kama hizi huwasilishwa katika lugha za kigeni kama Kiingereza. Kuna pia makanisha yanayopeperusha ibaada mitandaoni kama *Facebook* na ibaada hizi hupeperushwa katika Kiingereza au lugha nyingine za kigeni ili kufikia hadhira za kimataifa. Hali hii huathiri lugha za Kiafrika si kwa kuzifanya duni tu na kufisha moyo wazungumzaji wake, bali pia kwa kuzinyima nafasi ya kutumika katika mawasiliano ili kujiendeleza.

Dhima ya Kuhifadhi Lugha za Kiafrika

Maangamizi na hatari inayokumba lugha za ulimwengu imewafanya wataalamu wengi kupendekeza juhudi za haraka za kuokoa lugha hizi (Fishman, 1991; Paulston, 1994; Yamamoto, 1998; Crystal, 2000; Hinton & Hale, 2001; UNESCO, 2003; Grenoble & Whaley, 2006). Juhudi za kuokoa lugha ni za dharura kwa kuwa lugha zinaangamia haraka mno ilhali kila lugha ina manufaa mengi kwa jamii (Moseley, 2010; Prah, 2006; Reyhner, 1999; Sithole, 2001; Sommer, 1992; Sure, 2006). Krauss (1992) anasema kwamba juhudi za kuokoa lugha sharti zianze na jamii yenyewe. Uhifadhi wa lugha huwa na manufaa mengi.

Lugha hutambulisha watu. Lugha ya mama ya mtu ndiyo inayoweza watu wengine kubaini anakotoka. Mathalani, Kiswahili husaidia watu wa mataifa ya Afrika Mashariki kutambulika wanapokuwa nje ya Afrika Mashariki. Katika kila taifa, lugha mbalimbali hutumika kubaini asili ya kila mtu. Kwa hali hiyo, kuangamia kwa lugha zao, kutasababisha kupotea kwa utambulisho wa watu.

Lugha si njia ya kuwasilisha mawazo na hisia tu. Lugha pia huwasilisha utamaduni wa jamii. Lugha hutumika kufafanua mazingira ya jamii inayoizungumza. Hakuna lugha nyingine iliyo na uwezo huu. Lugha hutumika kutunga na kuwasilisha nyimbo za jamii ambazo ni sehemu ya utamaduni wake. Lugha hutumika katika dini, katika ibaada na mawasiliano ya maabadani. Dini ya jamii hutegemea lugha ya jamii hiyo. Lugha hutumika kuwasilisha hadithi za jamii ambazo ni sehemu ya amali muhimu ya jamii. Kwa hivyo, lugha ni nguvu zinazishikilia jamii pamoja na kuiunganisha na historia yake.

Watu wanaozungumza lugha moja huwa na mshikamano. Lugha huwafanya wazungumzaji wake kuwa na uhusiano wa karibu. Lugha huwafanya kufikiria pamoja na kukabili changamoto zao kwa pamoja. Ukosefu wa lugha moja huifanya jamii kusambaratika. Lugha za Kiafrika huwafanya Wafrika kuwa wamoja katika misingi ya kila jamii. Maangamizi ya lugha hizi yanaweza kuwa tisho kubwa kwa umoja wa Waafrika.

Utegemezi wa lugha za jamii jirani husababisha wazungumzaji wa lugha kupoteza hadhi zao. Lugha huwapa wazungumzaji thamani kama wanadamu na utegemezi wa lugha hushusha thamani hii. Matumizi ya lugha za kigeni katika nyanja zote yamesababisha Waafrika kuonekana kama wakosa lugha. Ni uhifadhi na matumizi tu ya lugha asilia za Kiafrika yatakayorudisha hadhi hii.

Maendeleo ya jamii katika nyanja zote hutegemea mawasiliano. Wanadamu hutagusana katika njia nyingi katika harakati zao za kuleta maendeleo. Mitagusano hii huhitaji mawasiliano yanayotegemea lugha. Ujumuishaji wa watu katika michakato ya kuleta maendeleo hutegemea ufanisi wa mawasiliano. Katika bara la Afrika, hili huhitaji lugha za wanajamii kwa kuwa ndizo hutumiwa mno katika mawasiliano hasa katika maeneo ya mashambani. Hii ndiyo sababu Feather (2003) anasisitiza kwamba uhifadhi wa lugha asili za jamii ndiyo njia ya pekee ya kuwahusisha katika maendeleo ya kiuchumi, kielimu na kijamii.

Kuhusu haki za lugha, wataalamu wengi wa lugha sasa wanashikilia kwamba kila mwanadamu ana haki ya kuwa na lugha mama (Thondhlana, 2002; Prah, 2006). Hii ina maana kwamba haki za lugha ni haki za kibinadamu kama tu haki nyingine. Azimio la UNESCO la Harare la mwaka wa 1997 kuhusu sera za lugha barani Afrika lilitambua haki hii muhimu na kuisisitiza kuhusu umuhimu wa kuheshimu haki hii (Thondhlana, 2002). Kwa hivyo, mtu anayekosa lugha mama huwa amekosa haki muhimu na anayenyimwa lugha huwa amenyimwa haki ya kimsingi.

Njia za Kuhifadhi Lugha

Sababu moja kuu ambayo imesaidia kuimarisha lugha ulimwenguni ni matumizi katika elimu. Lugha zinazotumiwa kama lugha za elimu huimarika bila kutishiwa na maangamizi. Mathalani, Kiingereza na Kifaransa zimetawala ulimwenguni kutokana na nafasi iliyochukuliwa na lugha hizo kama lugha za elimu katika mataifa mengi ya ulimwengu. Barani Afrika, lugha hizi zimetawala kutokana na matumizi yake kama lugha za mafundisho. Jukumu hili linaweza kutekelezwa pamoja na lugha nyingine za Kiafrika kama hatua ya kuzihifadhi lugha hizo.

Baadhi ya dhima za mawasiliano zinaweza kutekelezwa na lugha za Kiafrika. Mawasiliano ya shuleni yanaweza kuwa huru na ya kushirikisha lugha zote za wanafunzi. Hii ina maana kuondoa sera za kibaguzi za shule zinazolazimu matumizi ya Kiingereza na lugha nyingine za kigeni pekee katika mawasiliano ya shuleni. Panaweza pia kuwa na sera ya ufundishaji wa lugha za Kiafrika shuleni. Hili litatekelezwa kwa kuwapa wanafunzi kuteua lugha ya Kiafrika ambayo itafundishwa pamoja na Kiingereza na Kiswahili. Hapa, wanafunzi wanaweza kujifundisha lugha zao za mama au lugha za maeneo.

Sera ni muhimu katika uhifadhi wa lugha. Lugha zisizo na majukumu maalum kisera hujikuta zikitekeleza majukumu machache huku zile zilizo na majukumu kisera zikinawiri. Lugha zilizo na majukumu machache hufifia kidhima na wazungumzaji wake kuhamia lugha zilizo na majukumu ya kisera. Hali hii huwa hatari kwa maisha ya lugha na inaweza kusababisha maangamizi yake. Majukumu ya kisera yanaweza kulenga kuipa lugha dhima katika masuala ya uchumi, siasa, utawala na mawasiliano. Majukumu kama haya husaidia kuhifadhi lugha kwa kuiendeleza katika mawasiliano. Mathalani, nchini Afrika Kusini, kuna lugha kumi na moja ambazo zimepewa jukumu la kuwa lugha za rasmi. Sera hii imekuwa na nafasi kubwa katika uhifadhi wa lugha hizi.

Vyombo vya habari navyo vina nafasi kubwa katika uhifadhi wa lugha. Matumizi ya lugha katika vyombo vya habari ni njia muhimu ya kuinua hadhi ya lugha. Vyombo vya habari huwa na usikilizaji mpana unaoweza kutumiwa kama njia ya kuwashirikisha watu katika mawasiliano yanayohusisha lugha mama zao. Vyombo vya habari huwa na vipindi vya mazungumzo ya kidayalojia inayoshirikisha mashabiki kupitia kwa simu. Hii ni njia muhimu inayoweza kusaidia kuendeleza lugha kupitia kwa mawasiliano. Vyombo vya habari pia hushirikisha nyimbo zilizo katika lugha za mama. Nyimbo ni njia muhimu inayoweza kutumiwa katika ujifundishaji na upokezaji wa lugha za Kiafrika. Nchini Kenya, kuna vyombo vingi vya habari vinavyotangaza katika lugha za Kiafrika kama Mulembe FM, Redio Ramogi, Changei FM, Radio Mayienga, Musyi FM. Kitwek FM miongoni mwa vingine. Vyombo hivi hutekeleza jukumu kubwa katika upokezaji na uhifadhi wa lugha.

Uhifadhi wa utamaduni ni muhimu katika uhifadhi wa lugha. Uhifadhi wa lugha haiwezi kutenganishwa na uhifadhi wa utamaduni. Lugha na utamaduni ni vitu vilivyofungamana. Lugha hutumiwa kuwasilisha utamaduni wa jamii inayozungumza lugha hiyo. Lugha pia ni sehemu ya utamaduni wa jamii. Baadhi ya masuala ya kitamaduni hayawezi kuwasilishwa kupitia kwa lugha nyingine ila lugha ya jamii husika. Vipengele vya utamaduni kama fasihi simulizi haviwezi kuwasilishwa kwa kutumia lugha nyingine. Kwa sababu ya kufungamana kwa lugha na utamaduni,

uhifadhi wa lugha unapaswa kwenda sambamba na uhifadhi wa utamaduni wa lugha hiyo. Iwapo utamaduni utahifadhiwa, jamii itaweza kuhifadhi upekee wake pamoja na utambulisho na uhifadhi wa lugha utarahisishwa kutokana na jamii kujitambua kitamaduni.

Maandishi pia ni njia muhimu ya kuhifadhi lugha. Lugha inapokuwa na machapisho, huwa na uwezekano mkubwa wa kuamshwa hata inapoelekea kuangamia. Sababu huwa kwamba sarufi na msamiati wake upo na unaweza kuanza tena kutumika katika juhudi za kuiamsha lugha hiyo. Machapisho yanaweza kuhusisha vitabu vya fasihi, sarufi na kamusi. Machapisho yaliyo katika mitindo mbalimbali ikiwemo mitandaoni inaweza kutumiwa katika usomaji na ujifundishaji wa lugha. Vizazi vipya visivyo na uwezo wa kutagusana na wanajamii kutokana na uhamaji vinaweza kutumia machapisho kupokezwa au kujipokeza lugha za mama.

Utafiti kuhusu lugha pia ni njia muhimu ya kuhifadhi lugha hiyo. Utafiti hulenga kuhifandi msamiati wa lugha kabla ya kutoweka. Lugha zilizo katika tisho la kuangamia hupoteza msamiati kwa haraka kupitia kwa uhamaji lugha. Msamiati unaowasilisha utamaduni wa jamii hupotea kwa haraka na juhudi za uhifadhi zinahitaji kuhusisha utafiti wa kupata msamiati kama huu. Tafiti kama hizi kutamatia katika uchapishaji wa kamusi zinazoweza kutumiwa kuamsha lugha inayoangamia. Tafiti hizi zinaweza kuhusisha watalamu wa lugha wakishirikiana na serikali.

Mitandao na intaneti kwa ujumla imeibuka kama njia maalum na maarufu ya mawasiliano. Kuna mitandao mingi inayotumiwa katika mawasiliano ya kirafiki kama Twita, Watsapu, Instagramu na Facebook. Mitandao hii, hususan ile inayotumiwa na halaiki kama Facebook inaweza kuwa na manufaa makubwa katika mawasiliano yanayohusisha lugha za Kiafrika. Kadhalika, intaneti inaweza kutumiwa kusambaza vitabu na kamusi zilizochapishwa katika lugha za Kiafrika. Mitandao na intaneti, kwa hivyo, inaweza kutumiwa kama darasa la kujifundisha lugha za Kiafrika au jukwaa la kupata marejeleo na msamiati wa lugha hizi.

Machapisho pia yanaweza kuchukua mtindo wa mabango. Hii ni njia ya kutumia ilani kupasha watu misemo, methali, mafumbo au amali nyingine za kitamaduni ambazo zinaweza kuamsha ari ya kujifundisha lugha. Mabango haya yanaweza kuwekwa katika maeneo mengi ya barabara za jamii. Mabango yanaweza pia kuwekwa katika shule na maeneo ya maabadi ili kuonekana na kusomwa na watu wengi. Mabango pia yanaweza kuangikwa katika mitandao iliyo na wazungumzaji wengi wa lugha fulani kama njia ya kuwafikia kupitia kwa intaneti.

Hitimisho

Utandawazi umekuwa na athari kubwa kwa lugha. Umesababisha tisho kubwa kwa lugha zizizo na nafasi kubwa katika mawasiliano. Utandawazi umeathiri elimu, uchumi, mawasiliano, siasa na hata utamaduni. Athari hii imeathiri lugha kwa kuwa usambaji wa utandawazi umesababisha matumizi ya lugha chache za ulimwengu huku lugha nyingine zikipuuzwa na kuwa katika tishio la maangamizi. Juhudi kubwa zinapasa kufanywa ili kuokoa lugha hizi. Juhudi hizi zinaweza kujumuisha matumizi katika elimu, utawala na intaneti. Juhudi pia zinapasa kufanywa kuweka sera itakayohakikisha uhifadhi wa lugha hizi. Uhifadhi wa lugha hizi ni muhimu kwa kuwa lugha huwasilisha utamaduni, hutambulisha watu na sehemu muhimu ya amali zao.

Marejeleo

- Abari, A.O., Oyetola, I.O., Okunuga, A.A. (2013). Preserving African Languages and Territorial Integrity in the Face of Education and Globalization. *Problems of education in the 21st century Volume 57*, 2013 11 ISSN 1822-7864
- Archibugi, D., Lundvall, B. A. (Whr), (2001). *The Globalising Learning Economy*. Oxford: Oxford Univ. Press
- Batibo, H.M. (2005). *Language decline and death in Africa, causes, consequences and challenges*. Cleveland: Multilingual Matters.
- Chimerah, R. (1998). *Kiswabili: Past, Present and Future Horizons*. Nairobi: Nairobi University Press.
- Chiraghdin, S. na Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswabili*. Nairobi: O.U.P
- Crystal, D. (2000). *Language Death*. Cambridge: CUP
- Feather, J. (2003). *Communicating knowledge: publishing in the twenty first-century*. K. G. Saur: Mnchen

- Fishman, J.A. (1992). *Revising Language Shift: theoretical and foundations of assistance to threatened language*. Clevedon: Multilingual Matters
- Gerard, A. (1981). *African Language Literatures: An introduction to the Literary History of sub-sabara Africa*. Harlow: Longman.
- Githiora, C. (2006). *Kenya: language situation*. London: Elsevier
- Guerrieri, P. (1999). Patterns of national specialisation in the global competitive environment, katika: D. Archibugi, J. Howells, J. Michie (whr.), *Innovation Policy in a Global Economy*, Cambridge Cambridge: Univ. Press.
- Hinton, L. na Hale, K. (2001). *The green book of language revitalization in practice*. Sandiego: Academic Press.
- Jennings, J. (2011). *Globalizations and the ancient world*. Cambridge University Press.
- Khatib, M. S. (1983). Historia na maendeleo ya Kiswahili Zanzibar. Katika TUKI, *Lugha ya Kiswahili: makala zasedmina ya kimataifa ya waandishi wa Kiswahili 1*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
- Krauss M. (1992). The Worlds Language in Crisis. *Language* kur. 68: 4-10
- Marcel, B. (1983). Lugha ya Kiswahili nchini Burundi. Katika TUKI, *Lugha ya Kiswahili: makala zasedmina ya kimataifa ya waandishi wa Kiswahili 1*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kur. 55-61.
- Mazrui, A.A. na Mazrui, A. (1995). *Kiswahili State and Society: the Political Economy of an African Language*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mbaabu, I. (1078). *Kiswahili Lugha ya Taija*. Nairobi: K.L.B.
- McLaughlin, E.S. (2008). Language, democracy, and governance in South Africa. Webb, V. & du Plessis, T. (Whr), *The politics of language*. Arcadia, Pretoria: Van Schaik Publishers, kur. 118-137.
- Chakava, H. (1996). *Publishing in Africa: one man's perspective*. Nairobi: East African Educational Publishers, Ltd.
- Mkuthuria, M. (2009). Islam and the Development of Kiswahili. *Journal of Pan African Studies Vol 2 no 8* kur. 36-45
- Moseley, C. (Mhr.). 2010. *Atlas of the world's languages in danger*. Toleo la Tatu. Paris: UNESCO Publishing.
- Otieno, J. (2010). *The East African*, Nov 18, 2010. Nairobi: Nation Media Group.
- Paulston C. B. (1994). Social factors in language maintenance and language shift.in Pausto katika C. B. Pauston na wengine (1994). *Linguistic minorities in multilingual settings, studies in bilingualism* 4. Philadelphia: John Benjamins.
- Prah, K.K. (2006). *Challenges to the promotion of indigenous languages in South Africa*. Inapatikana http://www.casas.co.za/FileAssets/NewsCast/misc/file/204_CV_Challenges%20to%20the%20Promotion%20of%20Indigenous%20Languages%20in%20Sou_.pdf
- Reyhner, J. (1999). Some basics of indigenous language revitalization. In: Reyhner, J., Cantoni, G., St. Clair, R. N. & Parsons Yazzie, E. P. (Whr), *Revitalizing indigenous languages*. Flagstaff, AZ: Northern Arizona University, kur. v-xx.
- Shabani, M. H. (1983). Lugha ya Kiswahili nchini Rwanda. Katika TUKI, *Lugha ya Kiswahili: makala zasedmina ya kimataifa ya waandishi wa Kiswahili 1*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kur. 51-54
- Sithole, J. (2001). *African indigenous languages endangered*. inapatikana http://www.afrol.com/Categories/Culture/cul014_languages_die.htm
- Sommer, G. (1992). A survey on language dearth in Africa. Katika Brenzinger, M. (Mhr.), *Language death: factual and theoretical explorations with special reference to East Africa*. Berlin: Mouton de Gruyter, Kur. 303-314.
- Sure, K. (2006). English language teaching and identity crisis in Africa: illustrations from Kenya. Katika: Mutasa, D.A. (Mhr.) *African languages in the 21st Century: the challenges*. Brooklyn Square, RSA: Simba Guru Publishers, kur. 13-45.
- Thondhlana, J. 2002, Using indigenous languages for teaching and learning in Zimbabwe. In: Burnaby, B & Reyhner, J. (Whr), *Indigenous languages across the community*. Flagstaff, AZ: Northern Arizona University, Kur. 31-39.
- UNCTAD, (2001). *World Investment Report, Promoting Linkages*. Geneva: United Nations.
- UNESCO (2003). *Language vitality and endangerment*. Inapatikana <http://portal.unesco.org/culture/en/ev.php-url=9105>
- Yamamoto A.Y. (1998). *Respect and prospect on new emerging language communities*. London: Foundation for Endangered Languages.

